

Penda Kijiji Chako!

Inasikitisha jinsi ambavyo watu huamini kuwa Mungu amekuja kuwaangamiza. Watu humwona Mungu kama aliye na uweza wote na anayesubiri kuwahukumu na kuwaangamiza wanadamu. Watu hawa wanapasa kuangalia. Mathayo 23:37;

“Ee Yerusalemu, Yerusalemu uwauwaye manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako, kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mabawa yake, lakini hamkutaka.”

Yesu aliangalia mji wa Yerusalemu na akakumbuka dhambi za watu. Aliyaona maovu yote waliyoyafanya. Ijapokuwa waliwaua wale waliotumwa na Mungu, aliwahurumia na hata akataka kuwakusanya pamoja.

Je, Yesu alikuwa na hasira? Je alitaka kuangamiza mji wa Yerusalemu? La! Alijaa huruma kwa watu wa Yerusalemu. Mara nyingi katika Vijiji vyetu tunawachukia ‘wenye dhambi’ – watu wanaoshikilia msimamo na imani tofauti. Tunawahukumu na kuwatenga. Wakati mwingine tunawafukuza makanisani na vijijini mwetu. Hii si tabia na dhamira ya Yesu.

Aliwaona kama watu waliohitaji msaa kama vifaranga. Kabla mayai hayajaanguliwa kuku huyalalia ili kuyatia joto. Vifaranga wanapokuwa wachanga kuku huwalisha na kuwaficha chini ya mbawa zake. Hivyo ndivyo alaiyo Yesu kwa watu wake.

Licha ya kwamba tumetenda dhambi, Mungu anataka kutufahamu na kutujali. Mfuasi mkuu wa Yesu, Mtume Paulo, alisema haya kuhusu upendo wa Mungu:

“Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.” (Warumi 5:8)

Mungu hakungoja tuwe wazuri. Alitufia tukiwa wenye dhambi. Ikiwa Yesu hakutuacha na kututupilia mbali, basi tuna haki gani kufanya hivyo kwa wengine? Yesu alituhurumia na hivyo ndivyo itupasavyo kufanya kwa wengine na kwa wote walio karibu nasi. Tunahitaji kupenda na kujihusisha katika Vijiji vyetu, na si vinginevyo!

Zingatia!

Tengeneza orodha ya kila mmoja ambaye wewe au Kijiji kimembagua na kumtenga na uwaombee. Jaribu kutafuta njia za kuwabariki – chukua muda wa kufahamiana nao. Kwa njia hii utapata nafasi nzuri ya kuonyesha upendo na huruma kwao.


Omba:

- 1) Watu wataona upendo wa Mungu uking’aa kupitia kwao.
- 2) Unaweza kujaa huruma kwa ajili yao.



“Mahali tunakoishi tulikuwa karibu na umaskini na hatukusaidiana. Mungu ametusaidia sana kwa kutuletea Shirika la Dignity katika Kijiji chetu. Shirika hili limenisaidia kuongoza kanisa langu vyema zaidi.”

- Myombo, Lubwe, Zambia



Somo hili limedhaminiwa na, “Mungu ni Pendo” somo linalopatikana katika kitabu cha “Kipende Kijiji Chako” Kinachopatikana hapa:

dignityonline.org.uk/publications